Yesu Ni Nani?

Kama vile mimi, kwamba tumekuwa na yubile ya ulaji bora sana, kufikia sasa, pamoja na kiamshakinywa hiki kizuri tulichokula; kwa kawaida ni kipande cha andazi baridi kilichozungushiwa jeli. Nilikuwa Phoenix, hivi majuzi, nao wakanipa magole bila...tunaziita, huko Kusini, "chapati-maji," wala hazikupakwa 'lasi yoyote, na kwa hiyo i—i—ilinibidi kuzitia zangu sukari. Zilikuwa tu...Na sasa, hapa, tulikuwa na wakati mzuri kweli! Na si hilo tu, hilo ni katika mambo ya kawaida, tuna mmoja katika mambo ya kiroho.

2 Nina furaha sana kuusikia ushuhuda wa maskini ndugu huyu. Niliitwa hivi majuzi asubuhi kando ya kitanda chake; waliniambia jambo fulani lilikuwa limetukia. Nafikiri alikuwa ni mmoja wa wale wa kwanza waliojaribu kuudhamini mkutano huu. Hakika Shetani ndiye aliyejaribu kumfanyia hivyo huyo mtu wa Mungu. Lakini mnaona jinsi Mungu afanyavyo, Yeye huligeuza moja kwa moja likawa ushuhuda wa ajabu sana, kuonyesha nguvu Zake. Yeye atafanya kila kitu kitende kazi kwa manufaa, kwa wale wampendao. Ninashukuru sana kuusikia ushuhuda huo, ndugu.

3 Na kwa kweli imekuwa ni majaliwa kwangu kuwa katika jiji hili, pamoja nanyi watu. Ni, mbona, kamwe siwezi kulielezea, jinsi ninavyojisikia kulihusu. Sasa hatujakuwa na umati wa kufurika, na kadhalika, kama tunaokuwa nao wakati mwingine; lakini inaonekana kana kwamba Mungu anajiandaa kufanya jambo fulani, ama kitu fulani kinaimarishwa, kuwafanya tu watu tayari kwa ajili ya jambo fulani, kuwarudisha watu mstarini ambapo wanapaswa kuwa, na kukutana na wachungaji hawa wazuri, na kadhalika.

4 Na, basi, majaliwa yangu kuja hapa asubuhi ya leo kuwahubiria Wafanya Biashara wa Full Gospel. Nasikia ya kwamba tawi hili la hapa lingali changa. Ni dogo sana, na ni kama vile ndugu alivyosema hapa kwamba wanawahitaji watu.

5 Vema, licha ya idadi kubwa ya mashirika makubwa mazuri kama—kama niliyowakilisha kote ulimwenguni, yote ya full Gospel, mengi ya Wabaptisti na mengine mbalimbali, mbona, ningali ni mwanachama wa kundi moja, na hilo ni la—la Wafanya Biashara, kwa maana haliwakilishi dhehebu lolote lile. Lenyewe, ni—ni la baina ya mashirika ya Kiinjilisti. Kwa kifupi haliwakilishi chochote ila tu ni Injili yote, na kwa hiyo tunafurahia hilo.

6 Nami nafikiri ya kwamba, ninyi hapa watu wa mjini, ambao...Kwa kweli, kama mnaniamini kuwaambia jambo ambalo ni kweli, huu ndio wakati ambapo hao wafanya biashara

wa full Gospel wanapoweza kukusanyika pamoja kwa ajili ya ushirika. Mtajifunza mambo ninyi kwa ninyi, katika wakati kama huu Jumamosi asubuhi, kuzungumza.

7 Rais wa...rais wa kimataifa, Ndugu Shakarian, alitambulishwa kwangu miaka mingi iliyopita. Wengi wenu mnajua kuhusu hilo, juu ya nyaraka za telegramu kwenye dawati, lundo kubwa hivi; na nikitwaa kutoka mle, nilimpata mwanamke jina lake Shakarian, akifa kwa kansa. Na kwa namna fulani Bwana akaniongoza huko, na huko ndiko nilifahamiana na akina Shakarian, wakati alipoponywa. Hapo ndipo Daktari Theodore Palouveas alipobatizwa huko nje, wakati, yeye akiwa ni daktari wao, daktari Myunani.

8 Yeye alisema, "Wazo lenyewe, wewe ukiwaimarisha watu chini ya dhana ya uongo." Kasema, "Mwanamke huyo amelala pale akifa!"

9 Kwanza, wakati nilipoingia nyumbani, alisema, "Sasa utakapoingia," kasema, "uwe na kicho, mtulivu," kasema, "kwa kuwa mwanamke huyo yuafa. Amekuwa hapa juu, na matiti yote mawili yamekwishaondolewa, naye amevimba sana." Kasema, "Hana budi kufa." Kisha kasema, "Hakuna kitu unachoweza kufanya juu yake." Nami nikasikiliza tu hotuba yake kwa kitambo kidogo. Akasema, "Sasa kuwa mtulivu kabisa. Usiombe kwa sauti kubwa au chochote kile." Kasema, "Omba dua yako ndogo kisha urudi huku."

Nikasema, "Naam, bwana."

10 Kwa hiyo nikaendelea. Nilijua sikuwa ninaenda kuyasikiliza hayo, mwajua. Nami nikasema sisi...Nikapanda juu. Na kulikuwepo, ninaamini nilichukua...Niliichukua tena sasa. Nikapanda juu. Naye Florence, hapo, maskini msichana mdogo, mrembo, na Rose na wote hao, wote wakiomba; naye mama yao amelala pale hajifahamu, alikuwa amepoteza fahamu siku kadhaa, amevimba sana.

11 Na kwa hiyo nikapiga magoti kuomba. Na nilipofanya hivyo, hapo akaja Malaika wa Bwana, akaja chini kitandani, kasema, "Katika siku tatu ataamka."

12 Kwa hiyo nikageuka tu na kuanza kutoka, nao wakanifuata. Nikasema, "Katika...Ni katika Jina la Bwana, ataamka." Na basi wakaanza kupiga mayowe.

13 Huyu hapa akaja Daktari Palouveas, naye alikuwa akitaka kunifukuza kutoka kwenye nyumba hiyo. Naye akaninii tu... Nikasema...Akasema, "Wazo lenyewe!" Nami nikasema... "Vema, kuwaimarisha hao watu chini ya matumaini ya uongo! Mwanamke huyo yuafa."

14 Nikasema, "Kulingana na takwimu zako zote, ni hivyo. Lakini kulingana na Neno la Bwana, hapana." Mnaona? Nikasema, "Ataishi."

15 "Upuuzi," akasema, "unapaswa kuondoka mahali hapa, toka hapa."

16 Ndipo Ndugu Shakarian akakaribia, akasema, "Hebu kidogo." Unaona? Kasema, "Tulikuwa na wewe hapa chini, pia, kama daktari wetu, nasi tunakuthamini." Kasema, "Lakini pia tulimwita Ndugu Branham. Matumaini yako, hukutupa yoyote. Yeye anatupa, unaona."

17 Ndipo nikasema, "Hebu niwaambie nitakalofanya. Kama hajaamka na ni mzima tena, katika siku tatu, nitaweka alama mgongoni mwangu, 'nabii wa uongo,' nasi tutaenda moja kwa moja hapa Los Angeles, nawe uingie kwenye gari lako, ushuke barabarani, ukipiga honi, ukinielekezea kidole, unaona. Na kama akiamka, acha niweke alama mgongoni mwako, 'daktari bingwatapeli,' na niingie kwenye gari lako na kupiga honi, unaona." [Kusanyiko linacheka—Mh.] Asingefanya hivyo. Baadaye, alibatizwa kwenye handaki la unyunyuziaji maji, naye alikuwa akimtumikia Bwana. Tangu wakati huo, yeye ametwaliwa Nyumbani Utukufuni.

18 Na kwa hiyo nikafahamiana na akina Shakarian. Baadaye nilikuwa mmoja wa waliowasaidia kuanzisha tawi lao la kwanza. Na kote nchini, kote ulimwenguni, nimewasaidia katika matawi yao. Wao ni kundi zuri sana la watu.

19 Nafikiri ya kwamba ninyi—ninyi mnapungukiwa na kitu fulani kwa kutofanya ushirika wenu uimarishwe hapa, kwa sababu ni ushirika. "Tunapaswa kukusanyika pamoja," Biblia inatwambia hayo, "kadiri tuonavyo ule mwisho ukikaribia; tusiache kukusanyika pamoja." Itaninii—haitafanya hivyo tu, itawaimarisha. Na, ninyi, nguvu zenu zitaliimarisha kanisa. Na lote ni . . . Wafanya Biashara wa Full Gospel si dhehebu la kujitenga, na kusema, "Hili ni kundi letu." Ni kwa ajili ya waaminio wote, kukusanyika pamoja. Na ni shirika tu la kanisa, mnaona, kanisa lenyewe, waaminio wa kiroho. Nami nafikiri ni—ni jambo kuu kama ninyi—kama mngefanya hivyo. Kwa namna fulani ni dogo, labda halininii . . .

20 Natumaini halisikiki la kukufuru. Lakini mtu fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, kwenye mkutano, alisema, mtu fulani alisema, "Aisee, wewe ni mhubiri."

21 Nikasema, "Vema, kwa namna fulani nadhani ni sawa." Kidogo na—nahofia ninayosema juu ya wahubiri, nikiwa karibu na watu wa Full Gospel.

22 Mwajua, baba ya—yangu alikuwa m—m—mpanda farasi. Aliwafunza farasi. Nilipokuwa mvulana mdogo, niliwazia, mwajua, nilikuwa naenda kuwa mpanda farasi, pia. Mnajua jinsi wavulana wadogo wanavyopenda kuwa kama baba yao, nami nitakuwa mpandaji pia. Kwa hiyo ningempeleka baba nyuma ya mahali hapo, mwajua, wakati akilima, nami ningemchukua maskini farasi wangu wa kulima na kumpeleka kwenye kihori

cha kale cha kunyweshea, mwajua, kimechongwa kutokana na gogo.

23 Ni wangapi waliopata kukiona hicho, ninii cha kale... Vema, mnatoka sehemu gani ya Kentucky? Loo! Ni wangapi waliopata kulala kwenye godoro la manyasi? Vema, hata ni afadhali nitoe koti langu na tai yangu, kweli niko nyumbani hapa. Vema, hayo ni—hayo ni—hayo ndiyo mazingira yangu.

24 Kwa hiyo nilizoea kushuka kwenda huko chini. Naye baba alikuwa na tandiko, mwajua. Na kwa hiyo ningeweza kumwona huko mbali nyuma ya mahali pale, nami ningemchukua maskini yule farasi mkongwe wa kulima. Kisha nawachukua ndugu zangu wote, na kuwaweka kuuzunguka ua, mwajua, nami nilikuwa ndiye mwenye umri mkubwa zaidi ya hao tisa. Nikaenda nikaokota magugu mengi yenye miiba na kuyaweka chini ya tandiko hilo, na kuuvuta mkanda wa tandiko, kisha nikapanda juu yake. Jamani! Maskini jamaa huyo amechoka sana hata asingeweza kuinua miguu yake kutoka ardhini, naye aliguta tu na kufanya vituko, miiba ikimdunga, mwajua, huku nikimvuta kwa ule ukanda. Kwa hiyo ningeitoa kofia yangu, nami nilikuwa ninii tu...Nilikuwa kaoboi halisi. Nilikuwa nimesoma magazeti mengi kupita kiasi, hiyo tu. Kwa hiyo niliwafanya ndugu zangu kuamini nilikuwa kaoboi halisi, unaona, kwa hiyo nilidhani nilikuwa.

25 Nilipofikia kwenye umri wa kama miaka kumi na minane, nilitoka kisiri nyumbani nikaenda Arizona. "Walinitaka nikawafunze farasi wao. Nina hakika na jambo hilo. Walininii tu...Walinihitaji, kwa hiyo sina budi kuondoka nyumbani." Nikiwa na umri mdogo, lakini niliondoka kisiri, ndipo ikatokea kwamba nikafika Phoenix kwa wakati mzuri wa mashindano ya kuwafunza farasi, mwajua. Kwa hiyo nikaenda kule nyuma kuwaangalia mifugo yao vizuri, nione ni yupi nitakayempanda. Yule ambaye hao wengine wasingeweza kumpanda, nitampanda, mwajua, mwenye tandiko la fedha.

26 Nilikuwa jamaa mdogo, daima nimekuwa mdogo sana, nami nikafikiri ningejipatia jozi ya suruali ya ngozi. Ninajua baba yangu alizivaa. Naye hakuwa na yoyote wakati huo, na kwa hiyo nikajipatia...Niliona jozi zuri, mwajua, imeandikwa A-r-i-z-o-n-a hapo chini, vichwa vya maksai na kadhalika juu yake. Nikawaza, "Loo, jamani, hiyo itanienea vizuri," mwajua, jinsi ambavyo mtoto mdogo. Nikazivaa, takriban inchi kumi na nane zake zilikuwa sakafuni. Nami nilionekana kama mmoja wa hawa kuku wadogo, mwajua, wakiwa na hayo manyoya. Nikawaza, "Hiyo haitafaa kitu," kwa hiyo niliondoka tu nikanunua jozi ya Levis.

27 Nami nikawaza, "Nitapata fedha." Kwa hiyo nikaenda na kuwachunguza kwa makini hao mifugo waliokuwa

wamesimama pale, wakaidi sana hata wasingekula nyasi kavu, nazo zimewekwa horini. Nikawaza, "Loo, jamani!"

28 Kwa hiyo mara ya kwanza walipotolewa, ilitokea kuwa ni. . . Ajabu, nikisema hili asubuhi ya leo, kamwe sikuliwazia mpaka sasa hivi; lakini farasi wa kwanza kupandwa alasiri hiyo, kwenye mashindano, aliitwa "Haramia wa Kansas," na alitoka Kansas, haramia mkubwa mno wa urefu wa mikono kumi na saba kwenda juu. Na kwa hiyo huyu mpanda farasi mashuhuri pale alitarajiwa kumpanda.

29 Kwa hiyo nikasonga kwenye uzio wa zizi, kama wapandaji wengine, mnajua, na nikaketi pale juu. Wangeisukuma hii kofia nyuma. Nikawazia, "Ninaonekana kama mpanda farasi halisi," nikitazama juu.

30 Basi jamaa huyu akatoka, amepambwa kwelikweli. Yeye—yeye, wakati alibwagwa chini, kutoka kwenye farasi huyu, alifingirika kama mara mbili ama tatu naye huyo samaki wa madoadoa, na mvulana huyo. . . Farasi aliruka upande mmoja, naye huyo mtu akarushwa upande mwingine. Pikapu ilimchukua farasi. Nayo ambalansi ikamchukua mpandaji, damu ikitiririka kutoka masikioni mwake. Naye farasi akiteremka kule chini, nayo pikapu ikamchukua.

31 Huyu mwenye kuita akapitia pale na kusema, "Nitampa mtu yeyote dola mia moja atakayekaa juu yake sekunde kumi." Akatembea pale, akija kupitia pale, kasema, akanikazia macho, akasema, "Je! wewe ni mpanda farasi?"

32 Nami nikasema, "La, bwana." Nilibadilisha nia yangu, upesi sana. Kamwe sikuwa mpanda farasi.

33 Wakati nilipotawazwa kwa mara ya kwanza, Kanisa la Kimishenari la Baptisti, ningeibeba Biblia yangu kwenye kwapa langu, mwajua, namna *hiyo*, na nikapata hati za—zangu za utambulisho. Ni—nilikuwa mtetezi wa Imani, hakuna lingine. Nilidhani nilikuwa mhubiri.

34 Siku moja nilikuwako huku St. Louis, wakati huyu binti mdogo wa Daugherty alipoponywa, nami nilidhani nilikuwa ni mhudumu. Nilishuka nikakutana na Wapentekoste. Naye huyu Robert Daugherty, huenda baadhi yenu mnamfahamu. Nami nilimsikia akihubiri. Na mtu huyo alihubiri mpaka akaruka juu na kuyagonganisha magoti yake na kugeuka bluu usoni, kisha anashuka moja kwa moja sakafuni na kuruka juu tena, akikata pumzi, ungeweza kumsikia ukiwa umbali wa majengo mawili, angali akihubiri.

35 Mimi, njia zangu za polepole za Kibaptisti haziliwazii upesi jinsi hiyo. Mtu yeyote aliyeniambia, tangu wakati huo, "Je! wewe ni mhubiri?" Nasema, "La, bwana." Kwa namna fulani inanibidi kuangalia jambo hilo.

Jamaa fulani aliniambia, huko Filadelfia . . .

36 Huko ndiko mkutano ujao utakapofanyiwa, na wa kimataifa. Ninapaswa kuhubiri kwenye tarehe 29, nitaufungua mkutano huo tarehe 29, kwa ajili ya Daktari Brown na—na wengi wa hao ndugu huko. Huo ni huko Filadelfia, unaanza tarehe 29 mwezi huu. Ni majaliwa yangu kuufungua mkutano huo, kwa hiyo, na kuwa na viamshakinywa kadhaa kwa ajili yao.

37 Jamaa fulani alisema, "Kwa nini unaambatana na hilo kundi la Wafanya Biashara? Unajulikana kama mhubiri."

Nikasema, "Vema, mimi—mimi ni mfanya biashara."

Akasema, "Vema, unahusika na biashara ga—gani?"

38 Kisha nikasema, "biashara ya assurance [dhamana—Mh.]." Nikalitamka upesi sana asiweze kulishika, unaona. Hakupata nililosema. Kamwe sikusema "Insurance [bima]" nilisema "assurance [dhamana]."

39 Akasema, "Vema, nina—nina furaha ku—kujua hilo." Akasema, "Ninii, makao makuu ya kampuni hii yako wapi?" Kasema, "Ni bima ya aina gani?"

Nikasema, "Uzima wa Milele."

Akasema, "Kamwe sijasikia habari zake. Yako wapi makao makuu yake?"

Nikasema, "Utukufuni."

40 Hivyo yeyote wenu enyi jamaa ambaye anavutiwa, ningetaka kukuelezea hati yake baada ya ibada kumalizika.

41 Nami nakumbuka, wakati fulani uliopita, juu ya bima. Natumaini hakuna mtu wa bima hapa. Pamoja na hayo, Ndugu yangu ni mwuza bima, na Prudential. Kwa hiyo niliambiwa nilikuwa na bima iliyododa wakati mmoja. Nao hawakutusomea hati hiyo vizuri, basi baba kwa muda wa miaka kumi akalipia malipo ya miaka ishirini, malipo ya bima, tulidhani. Wakati ilipokuwa tayari kulipiwa, ilikuwa ina thamani ya dola saba na senti hamsini, nasi tulidhani ilikuwa ina thamani ya mamia ya dola. Lakini, na si—sijui. Ni sawa, bima ni sawa, sasa; siidunishi hiyo. Ni sawa kabisa.

42 Kwa hiyo nilikuwa na rafiki wa bima, ama aliuza bima, hasa, jamaa fulani niliyesoma naye; ndugu yake, yeye huandika kwenye *Chumba cha Juu*, ni mhudumu mzuri sana wa Kibaptisti. Kwa hiyo Wilmer alikuja kuzungumza na mimi, siku moja, kasema, "Billy, nimekuja kuzungumza nawe juu ya bima fulani."

43 Nikasema, "Vema, Wilmer," nikasema, "nitakwambia, daima tumekuwa marafiki wazuri," nikasema, "na kila kitu." Nikasema, "Ukitaka kuzungumza juu ya hali ya hewa, ama—ama kuhusu kitu kingine, vema, ila kuhusu kwenda kuwinda ama chochote kile. Niko radhi kuzungumza juu ya hayo. Lakini . . ."

Sasa akasema, “Vema,” kasema, “hakika unahitaji bima.”

Nami nikasema, “Ninayo dhamana.”

44 Naye akasema, “Loo samaha-. . .Basi nadhani Jesse,” huyo ni ndugu yangu, “tayari amekuuzia hati?”

45 Nikasema. “Hapana.” Na mke wangu akaniangalia kana kwamba nilikuwa mnafiki, unaona, maana alijua sikuwa na bima. Kwa hiyo akaniangalia. Nami nikasema, “Naam,” nikasema, “Nina dhamana.”

46 Kasema, “Ni ipi?” Nami nikasema:

> Dhamana iliyobarikiwa, Yesu ni wangu!
> Loo, ni kionjo cha jinsi gani cha utukufu wa Kiungu!
> Mimi ni mrithi wa wokovu, nimenunuliwa na Mungu,
> Nimezaliwa kwa Roho Wake, nikaoshwa kwa Damu Yake.

47 Akasema, “Billy, hilo ni zuri sana, bali hilo halitakuweka hapa juu kaburini.”

48 Nikasema, “Bali litanitoa. Mimi sina—mimi sina wasiwasi kuhusu kuingia mle; nina wasiwasi kuhusu kutoka humo.”

49 Enyi Wafanya Biashara, ningali katika biashara. Kama mkitaka kuzungumzia baadhi ya haya pamoja na mimi, nitafurahi kufanya hivyo nanyi.

50 Lakini ni jambo kubwa kuwa na ushirika. Ninaamini iliandikwa katika Maandiko, “Jinsi ilivyo vema na ya kupendeza kwamba ndugu wanaweza kukaa pamoja kwa umoja. Ni kama mafuta ya kutia yaliyokuwa ndevuni mwa Haruni, yaliyoshuka mpaka upindo wa sketi zake.” Kuna jambo fulani kuhusu ushirika!

51 Mungu peke yake, hapo mwanzo, Yeye alikuwa ni Mungu tu. . .Hata hakuwa ni Mungu, hapo mwanzo. Je! mlijua jambo hilo? Asingeweza kuwa. *Mungu* ni “kitu cha kuabudiwa,” neno la Kiingereza. Mnaona? Kama vile alivyokuwa Elohimu, Yeye anayeishi peke yake; hata hakuwa Mungu. Lakini ndani Yake mlikuwamo na sifa, kama vile mawazo yako. Mnaona? Wazo lako, sina budi kuona jambo fulani, na kisha. . .Ninaliwaza, na kisha kulinena. Nalo neno ni wazo lililodhihirishwa. Kwa hiyo, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, na Huyo Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno akadhihirishwa,” unaona, akatolewa.

52 Na sasa yote vile vile. Jinsi tulivyo, tumezaliwa mara ya pili, tuna Uzima wa Milele. Ikiwa tuna Uzima wa Milele, kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele, hiyo ni Mungu. Na sisi ni sifa Zake. Sasa ninaweza kuzungumza miongoni mwa Wakristo hivi. Sisi ni sifa. Naye Yesu alikuja kama Mkombozi. Ni wangapi wanaoamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kukomboa, si kuumba kitu kipya. Kukomboa

ni kukirejesha kile ambacho kimekuwako tayari. Unaona? Kwa hiyo unaogopeshwa na nini? Unaona? Yote—yote yako mikononi Mwake, saa haiendi vibaya. Kila kitu hakina budi kuwa jinsi hii, nalo linatuleta mahali hapa. Sasa . . .

53 Nami ninaamini na hakika ninatumaini ya kwamba kila mmoja wenu ninyi watu hapa asubuhi ya leo, ambaye si mshirika wa ushirika huu mzuri, ya kwamba utalizungumza hapa na mtu huyu mzuri; inanibidi tu kumpa mkono, ra—rais wa tawi hili. Basi jiimarisheni! Daudi alisema alijiimarisha mwenyewe dhidi ya adui. Nanyi watu, m—m—mnapaswa kufanya kila mwezacho kujiimarisha dhidi ya adui. Tuko hapa kama ndugu wa full Gospel, mnaona. Tunaiamini. Hebu na tuingie kazini, na tutoke na tukawatafute baadhi ya hawa ndugu wengine na kuwaingiza, wawe ni wa full Gospel ama sivyo, na kuwaingiza kwenye mikutano ye—yetu. Na tuombe na tutumikie sehemu yetu kuuimarisha Mwili wa Kristo, na, katika hilo, tunajiimarisha wenyewe. Mungu awe pamoja nanyi, awasaidie. Wakati wowote ninaoweza kuwafadhili, naomba mnijulishe. Sasa hebu sisi, kabla hatujalikaribia Neno . . .

54 Sitaki kuwaweka hapa muda mrefu sana. Ni—ninaninii tu . . . Kama nilivyosema muda mfupi uliopita, "Kwa namna fulani mimi ni mwenda pole, mwajua, na kidogo inanibidi kuliwazia polepole." Pia—pia si mwerevu sana, kwanza kabisa, kwa hiyo kidogo inanibidi kuchukua wakati wangu; wala sijui zaidi ya yale anayoniambia niseme, nalo huniingiza kwenye matatizo wakati mwingine, mara zingine hunitoa, kwa hiyo mimi husema tu kile Yeye asemacho. Lakini kabla hatujalikaribia Neno, hebu na tumkaribie Mwandishi.

55 Wakati fulani uliopita, nilikuwa nikiendesha gari na Daktari mashuhuri wa Uungu, huenda wengi wenu mkamjua, William Booth-Clibborn, naye huihubiri Injili katika lugha saba. Na tulikuwa tukizungumza juu ya Mungu na sifa Zake. Na nilikuwa nikizungumza kuhusu jambo hilo, kasema, "Ni kama vile almasi, ndivyo Mungu alivyo." Mnaona? Kisha nikasema, "Halafu karama hizi mnazonena habari zake," nikasema, "hizo ni—hizo ni uakisi tu wa upendo wa Mungu." Ndipo nikasema, "Kama vile huko Afrika, sisi . . . "

56 Rais wa migodi, huko Kimberley, alikuwa ni mmoja wa mababawabu wangu mstarini. Alinipitisha kwenye migodi ya almasi huko—huko Kimberley. Mbona, unaweza kuzipata barabarani, bali usithubutu kuweka moja isipokuwa iwe imekatwa. Haina budi kukatwa na shirika. Kwa hiyo basi almasi iliyo kubwa mno, haina moto ndani yake unapoipata. La, inapaswa ikatwe itoe moto.

57 Basi huyo alikuwa ni Mungu, Naye ilimbidi kujeruhiwa kwa makosa yetu, na kuchubuliwa kwa ajili ya maovu yetu. Yeye ni Almasi kuu. Halafu basi unapoikata almasi, (je!

ulipata kuona?) unaikata katika umbo la pembe tatu, nalo jua likiiangaza litaakisi rangi saba. Unaona? Na ukiangalia, nyekundu kupitia nyekundu, huonekana ni nyeupe. Ulipata kujua hilo? Hiyo ni kweli. Nyekundu kupitia nyekundu, hiyo ni Damu, Damu nyekundu ikiangalia ninii. . . Mungu akimwangalia mwenye dhambi mwekundu, kupitia Damu nyekundu, humgeuza mweupe. Yeye yumo ndani ya moyo, unaona.

58 Na—na kwa hiyo sasa, katika jambo hilo, nilisema, "Mungu alibambua, akakata, akachubua, kuakisi katika miali hii, inapolipiga Ne—Neno kuu la Mungu, linaakisi kile Mungu alicho."

59 Naye huyu Bw. Clibborn alisema, "Lakini wewe hujui tu Biblia yako."

60 Nikasema, "Hiyo huenda ikawa ni kweli. Ninamjua Mwandishi Wake vizuri sana. Kwa hiyo hilo—hilo ndilo jambo muhimu, kama ninamjua Mwandishi wake." Kumjua Yeye, iwe unalijua Neno lote, ama hulijui; kumjua tu Yeye!

61 Ninaamini ilikuwa ni Hudson Taylor aliyemwambia kijana mmishenari wakati mmoja. Akasema, "Bw. Taylor, ndiyo kwanza tu nimpokee Roho Mtakatifu," kasema, "je! niende nikajipatie Digrii yangu ya Sanaa?" Akasema, "Usijaribu kuangaza wakati mshumaa umetumika nusu. Hebu uangaze wakati ukiwaka." Kweli. Kwa maneno mengine, kama hujui la kusema, nenda ukasimulie jinsi ulivyowashwa. Hilo latosha.

62 Nanyi Wafanya Biashara wa Full Gospel fanyeni vivyo hivyo. Hai—haikubidi kungojea uwe mhudumu; wewe shuhudia tu kile Yeye amekufanyia tayari. Hicho ndicho kilichowafanya kuja pamoja hapa, ni kushuhudia kile ambacho amewafanyia. Hilo litaiangazia wengine Nuru wapate kuwashwa kwa hiyo. Hivyo ndivyo taa za maskanini zilivyowashwa, moja kutoka kwa nyingine; si nuru ya kigeni, kuwashwa kupya; bali ni nuru ile ile. Inamaanisha, ni Mungu yeye yule kotekote, anayeangaza hiyo Nuru.

Na tuzungumze na huyu Mwandishi mkuu sasa tunapoviinamisha vichwa vyetu.

63 Baba wa Mbinguni, kukusanyika pamoja sasa katika ulimwengu wa roho. Hili, tunatambua, si jengo la kanisa; hapana shaka ila Kiwanis na vilabu vingi mbalimbali, cha Lions na kila kitu, hukutana humu ndani. Lakini asubuhi ya leo ni kanisa kwa sababu wajumbe wa u—ule Ufalme wamekusanyika pamoja. Nasi tunajisikia, hata hivyo, tayari, kutokana na shuhuda hizi na nyimbo, tuna—tunauhisi Uwepo wa yule Mfalme mkuu. Tunajua ya kwamba Yeye yupo hapa.

64 Na sasa wakati sisi, kama watoto, katika kukutolea Wewe sifa za midomo yetu, loo, labda si kwa utaratibu, Bwana, lakini ni watoto tu, Wewe unaelewa hilo. Haidhuru tungejaribu jinsi

gani kutumia tabia ze—zetu na akili, huenda isitoke moyoni, ni kitu fulani cha kinafiki tulichojibandika. Lakini wakati sisi, kutoka moyoni mwetu, tunapokutolea heshima zilizoko humo kwa ajili Yako, nina hakika zitapokewa.

65 Sasa tunaomba ya kwamba utatufungamanisha tu kwenye kamba ya Roho Mtakatifu, uikusanye mioyo yetu pamoja, na kunena nasi kupitia Neno la Mungu.

66 Bariki tawi hili dogo, Bwana, ulipe nguvu. “Mimi Bwana nimelipanda, nitalitia maji mchana na usiku, asije mtu akalitoa mkononi Mwangu.” Ninaomba, Bwana, kama mtumishi Wako, wabariki. Watie nguvu, Bwana, kwa ajili ya Ufalme.

67 Bariki kila kanisa lililowakilishwa hapa ndani asubuhi ya leo, na kila mtu. Na kukiwako na wengine hapa asubuhi ya leo ambao—ambao kweli hawajaokoka, na—naomba, Mungu, ya kwamba hii itakuwa ndiyo saa ambapo wataona kwamba hawana uwezo kuyakabili mauti, kwamba watapokea ka—karama ya Uzima wa Milele kupitia Yesu Kristo Mwanao. Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake. Amina.

68 Sasa, katika mikutano, nafikiri nimewahubiria kwa nguvu sana na kila kitu, mikutanoni, sitaki kuchukua, kuhubiri somo. Nami ninafikiri kweli si sawa kuwa na m—mkutano bila ya kulisoma Neno, na kuzungumza kidogo tu juu ya Neno. Kwa hiyo hapa nimechagua kutoka kwenye Neno hapa, m—mchezo mdogo tu wa kuigiza, hadithi ndogo. Baadhi yenu, nimeisimulia mara mbili ama tatu, bali nafikiri ingefaa tena, mnaweza kunivumilia kidogo tu kwa jambo hili.

69 Nitaninii—nitasoma kutoka Kitabu cha Luka Mtakatifu, katika mlango wa 19, nikianzia kwenye kifungu cha 1. Ni maskini fungu dogo la kigeni sana, kuwazia juu ya kulileta mahali kama hapa. Lakini hata hivyo Neno lote limetiwa pumzi, linakaa vizuri mahali pake, na ninatumaini ya kwamba Mungu atalichukua Neno hili na kuliweka moja kwa moja mahali pake asubuhi ya leo.

> . . . *Yesu alipoingia Yeriko alipita katikati yake.*
>
> . . .*tazama palikuwa na mtu, jina lake Zakayo, mkubwa mmoja katika watoza ushuru, naye alikuwa ni tajiri.*
>
> *Huyo alikuwa akitafuta kumwona Yesu ni m—mtu wa namna gani,* . . .

70 Hebu nisome hilo tena, kwa sababu ninataka kulitilia hili mkazo.

> *Huyu alikuwa akitafuta kumwona Yesu ni mtu wa namna gani, asiweze* kwa sababu ya *umati wa watu,* ama *kwa sababu alikuwa ni mtu mfupi wa kimo.*
>
> *Akatangulia mbio, akapanda juu ya mkuyu apate kumwona, kwa sababu atakuja kupitia njia ile.*

Na Yesu alipofika mahali pale, akatazama juu, akamwona, akamwambia, Zakayo, shuka upesi, kwa sababu leo imenipasa kushinda nyumbani mwako.

71 Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Hili, Neno Lake.

72 Mtu huyu, mhusika mdogo, mandhari yetu inaanzia Ye—Yeriko. Sasa, Yeriko ulikuwa ndio mji ulio wa chini sana huko—huko Palestina, nao uko bondeni. Na—na Yerusalemu uko juu ya m—mlima, juu ya kilima.

73 Na kama uliona, Yesu, wakati alipokuja duniani, Yeye alipewa, miongoni mwa watu, jina duni sana angaliweza kupewa. Kuja Kwake, Yeye alikuwa "Beelzebuli," hilo lilikuwa ndilo jina baya kuliko yote wangaliweza kumwita, hilo ni, "ibilisi, mpiga ramli, pepo mchafu." Waliita kazi Yake pepo mchafu. Kanisa lisilokuwa tayari, kumlaki, walimpa jina baya sana, "Beelzebuli."

74 Naye alikuja, kuzaliwa kwa hali ya chini kabisa angaliweza kuzaliwa, na mama mkulima mdogo, hana hata mahali pa kulala chini a—apate kumzaa mtoto huyu. Na nguo Zake za kitoto, tunaambiwa, zilitolewa kwenye nira ya maksai, walizomfunikia, horini, katika zizi lililovunda, juu ya takataka kwenye zizi. Na zizi hilo hata si zizi lifaalo; pango dogo kwenye ubavu wa kilima.

75 Na Yeye alishughulika na watu wa hadhi ya chini kuliko wote, maskini kuliko wote. Naye alikataliwa na watu wa jamii ya hali ya juu sana kuliko zote. Alikataliwa na walio Wake Mwenyewe, kanisa ambalo lilipaswa kumjua, bali hawakumjua. Hawakufunzwa katika Neno, kumjua Yeye.

76 Na tunaona tena ya kwamba alienda kwenye mji wa chini kuliko yote uliokuwako Palestina, Yeriko. Ninasahau uko fiti ngapi chini ya usawa wa bahari, chini kabisa. Yeye alijishusha chini sana mpaka mtu aliyekuwa mfupi zaidi ya wote mjini ilimbidi kupanda juu ya mti kumwangalia akiwa chini.

77 Lakini hilo ndilo ulimwengu ulilowaza juu Yake. Walimpa kifo katili, kigumu sana ambacho mtu yeyote angeweza kufa; Yeye alikufa kama mhalifu. Kifo cha aibu sana angaliweza kufa, wakamvua nguo Zake; na, bila shaka, mnaona kwenye zile sanamu, na kadhalika, wamemzungushia kipande cha nguo. "Lakini aliidharau aibu." Walimvua nguo Zake zote, wakamsulibisha msalabani, katika aibu. Kifo cha chini kuliko vyote, kigumu kuliko vyote ambavyo vingeweza kutolewa, walimpa Yeye. Na hivyo ndivyo ulimwengu ulivyowaza kumhusu.

78 Lakini Mungu alimwazia hata akampa Jina lililo juu ya kila jina linalotajwa Mbinguni ama duniani. Akamwinua juu sana mpaka, kiti Chake cha enzi juu sana, inambidi kuangalia chini apate kuiona Mbingu. Hivyo ndivyo Mungu alivyomwazia. Nina hakika hayo ndiyo mawazo yetu asubuhi ya leo, pia. Liko juu ya

kila jina, juu ya kila jina linaloweza kutajwa. Hata familia yote Mbinguni na duniani inaitwa "Yesu." Na kwa Jina hili, kila—kila goti litapigwa, na kila ulimi utakiri Kwalo.

79 Zakayo alikuwa ni m—mfanya biashara tu katika mji wa Yeriko. Naye hapana shaka alikuwa ni mtu m—mzuri kwa njia yake. Yeye—yeye alikuwa, tuseme, ninaamini, kwa kuwa mtu mzuri kama alivyokuwa, hapana budi alikuwa ni mfuasi wa kanisa fulani, moja ya madhehebu ya siku hiyo. Hebu tuseme alikuwa ni Farisayo.

80 Naye, kweli, yeye hakukubaliana na maoni ya mke wake. Hebu tuseme jina la mke wake lilikuwa ni Rebeka. Naye hakukubaliana na maoni yake, kwa kuwa alikuwa amemwamini Yesu. Alimwamini kuwa kile alichokuwa hasa, Masihi, kwa kuwa alikuwa amemwona akifanya ishara ya Masihi. Yeye, akiwa ni Mwebrania; Waebrania huziangalia ishara na manabii, kwa sababu huyo alikuwa awe ni mjumbe wao. Hiyo ndiyo sababu hawakupaswa kamwe kushindwa kumfahamu, kwa sababu Yeye alikuwa anakuja, "Mwana wa Adamu."

81 Soma yaliyosalia ya mambo haya hapa yanayomhusu Zakayo. "Kwa sababu Mwana wa Adamu alikuja kuwatafuta na kuwaokoa waliopotea." Yeye ni Mwana wa Ibrahimu.

82 Hapo, walimshtaki kwamba anaambatana na wenye dhambi. Kwa hiyo tunaona walipaswa kuelewa hilo, bali hawakuelewa. Walikuwa na theolojia yao ya—ya kuishi maisha mazuri na kuwa watu wazuri, na kadhalika, lakini hawakuelewa kile hasa Masihi wao alipaswa kuwa.

83 Mnajua hilo lingeweza kutukia tena? Hilo lingeweza kutukia kwa urahisi sana, hata tungelielewa vibaya kwa njia fulani. Sasa kuna njia moja tu ya kuwa na hakika, hiyo ni, kutafuta kujua kile alichokuwa. Halafu, Maandiko yanasema, "Yeye ni yule yule." Tafuta kujua jinsi atakavyojidhihirisha Mwenyewe wakati wa mwisho. Imeandikwa. Mnaona, Yeye kamwe hafanyi lolote bila ya kulifunua kwanza. Alisema hivyo katika Maandiko, "Hafanyi neno, bila ya kuwafunulia watumishi Wake hao manabii." Naye amelifunua. Na *Hiki* ni nabii Wake, *Hiki* ni Kitabu cha unabii, ndicho ufunuo mkamilifu wa Yesu Kristo, kotekote. Hakuna kitu kitakachoongezwa, wala kuondolewa Kwake. Nasi inatupasa kukichunguza na kuona ni siku gani tunayoishi, maana huenda tukashikwa kwenye mtego ule ule.

84 Kwa hiyo tunaona ya kwamba kwenye wakati huu, ya kwamba huyu Zakayo, maskini mhusika wetu asubuhi ya leo, mfanya biashara huyu wa—wa Yeriko, sisi. . .huenda alikuwa ni mshirika wa Kiwanis, kama kulikuwako na kitu kama hicho, ama kitu cha kukiwakilisha. Hu—huenda alikuwa ni mwanachama wa chama kikuu kule, kilichokuwako Yeriko. Hapana shaka, mtu wa kipekee sana wa wakati wa—wake, naye alikuwa ni wa kanisa.

85 Lakini jambo baya tunaloona, ni kwamba alikuwa amekubaliana na maoni ya kisasa, maoni yanayopendwa na wengi, juu ya Yesu. Naye Yesu ni Neno; nalo Neno, linapodhihirishwa, ni Yesu. Unaona? Na kwa hiyo alikuwa amechukuliana na—na maoni yanayopendwa na watu wengi ya kwamba hakuwa ni nabii, ya kwamba alikuwa tu ni—ni—ni . . . Sitaki kulitaja neno hili, kama tunavyoweza kusema siku hizi, mwenye kujiinua, kitu tu kilichokuwa ni cha kuigiza.

86 Lakini, unaona, Shetani anaweza kuiga hilo kikamilifu sana mpaka ni vigumu kujua ni lipi la kweli na ni lipi la uongo. Yesu alisema ingekuwa hivyo katika siku za mwisho, uigaji mwingi sana, kama vile Yane na Yambre walivyoshindana na Musa.

87 Kumbukeni, hao watu wawili wangaliweza kufanya lolote ambalo Musa na—na Haruni wangaliweza kufanya. Lakini jambo pekee ambalo Musa alijua, na kuthibitishwa . . . Vema, kamwe hakuja, Yane na Yambre, kuwakomboa watumwa. Musa alikuja katika jina la Bwana, kuwakomboa watumwa, unaona, kwa maana ilikuwa imeandikwa hivyo. Walimwambia Ibrahimu, "Uzao wako utakuwa mgeni kwa muda wa miaka mia nne, bali nitawatoa." Kwa hiyo Musa alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Lakini wangeweza kuiga namna yoyote ya karama ambayo wangeweza kutoa. Wao wakijua hilo, kamwe hawakuwajali waigaji wao, walidumu moja kwa moja na Neno. Mungu hatimaye akatangaza.

88 Nanyi mnajua Yeye alisema ya kwamba ingekuwa katika siku za mwisho, "Kama vile Yane na Yambre walivyoshindana na Musa, ndivyo na watu hawa wenye akili potovu, kuhusu ile Kweli." Hiyo ni kweli, unaona, ni maigizo tu. Kwa hiyo kidogo huwa yenye kutatiza watu.

89 Wakati mwingine unawakemea, bali hata hivyo si—si kwamba huwapendi. Ni kwa sababu kweli unawapenda.

90 Vipi kama ulikuwa, mvulana wako mdogo alikuwa ameketi hapa nje katikati ya barabara, nawe ungetokea na kusema, "Mwanangu, mpenzi, sidhani inakupasa kuketi hapa nje"; angesema, "nenda kashike lako"? Ungempa ninii kidogo . . . Mnaiita nini, kama ile baba yangu aliyonipa? Kichemsha tako. Je! hivyo ndivyo, ndivyo linavyotamkwa? Hicho ndicho angehitaji.

91 Na kwa hiyo hicho ndicho huna budi wakati mwingine kulipa kanisa; sio kwa sababu humpendi Mwanao, bali ni kwa sababu kweli unampenda Mwanao. Unaona? Upendo husahihisha.

92 Hivyo, Yesu hakuwachukia. Aliwapenda, Naye hana budi kuwasahihisha.

93 Kwa hiyo tunaona maskini jamaa huyu na Rebeka, mkewe. Naye aliamini ya kwamba Yeye alikuwa ni nabii, yule Nabii. Hawakuwa na nabii kwa mamia na mamia ya miaka. Walijua

atakayefuata jukwaani, nabii wa halisi atakayefuata, angekuwa ni Yeye. Unaona, walijua huyo alikuja, maana ilitabiriwa. Kwa hiyo manabii walikuwa wamekoma, ndipo Yeye akajitokeza jukwaani. Naye alikuwa ameiona hiyo ishara ya Masihi, naye alijua hilo lilikuwa ni lile Neno. Mnaona, alikuwa amelichunguza kabisa.

94 Kwa hiyo mchezo wetu wa kuigiza unaanzia hapa. Hapana budi ulikuwa ni usiku mbaya sana kwa jamaa huyo mdogo. Ulikuwa usiku wenye usumbufu, na asingeweza kulala. Alikuwa—alikuwa akifingirika huku na huku, juu ya mto wake, usiku kucha. Wengi wetu wanajua kile usiku wa namna hiyo ulicho.

95 Unaona, Rebeka alijua. Alikuwa ana uhusiano na wale wanafunzi, na kadhalika. Alijua Yesu alikuwa aingie mjini kesho yake asubuhi. Naye alikuwa amehusika sana na mu—mumewe, hata alitaka akutanishwe uso kwa uso na Yesu. Na mtu anayewahi kusimama uso kwa uso na Yeye, linakufanyia jambo fulani. Yeye si kama watu wengine. Yeye ni tofauti. Naye alitaka kuhakikisha kwamba amemwona, ameona kazi Zake, na kujua ya kwamba Yeye alikuwa ni yule Masihi. Ingawa, makuhani na hao wengine walikuwa wamesema, "Hapana kitu hapo. Ni bandia tu. Ni—ni udanganyifu wa kimzaha." Lakini yeye aliliamini, kwa hiyo alikuwa akiomba.

96 Sasa, Rebeka, kama ukitaka kumleta mfanyabiashara wako, Zakayo, kweli mbele za Yesu, anza tu kuomba, atakuwa na wahaka.

97 Kwa hiyo wakati ulikuwa umekaribia, kwa hiyo, asubuhi iliyofuata, Yesu alikuwa apitie njia ile. Kwa hiyo usiku kucha akajipindua-pindua kitandani, na alikuwa mwenye mashaka. Naye mke, amelala pale, akiomba. Na bila shaka usiku huo, wakati wangeamka, angesema, "Asante, Bwana, ninajua unamshughulikia."

98 Sasa unapofikia kuona Zakayo wako hawezi kutulia, sema tu, "Asante, Bwana, Wewe unamshughulikia sasa." Unapomwona amejaa manung'uniko, hataki uende kanisani tena, unaona, "Kaa mbali na kundi hilo! Usishuke kwenda kule tena! Hakuna chochote kwa hilo!" Kuwa tu na subira. Mungu anafanya kazi, unaona. Hivyo ndivyo Yeye huifanya, unaona. Anahangaika sana hawezi kuvumilia.

99 Kwa hiyo tunaona, kesho yake asubuhi, mapema kabisa, maskini mhusika wetu anatoka kitandani kisiri na anaenda kujivika nguo zake zilizo nzuri kuliko zote, mwajua, vazi lake lililo zuri kuliko yote aliyokuwa nayo, na kuzichanua ndevu zake na nywele zake. Naye Rebeka anachungulia chini ya shuka na kumwona. Anajua papo hapo jambo fulani linaendelea. Kwa hiyo ananyemelea dirishani, na anaangalia aone kama mkewe anaangalia, kama yuko macho. La, hakuwa ameamka, kulingana

na alivyowazia. Analifungua pazia na kuangalia nje, na ilikuwa ni mapambazuko, kwa hiyo anajiandaa vizuri kabisa.

100 Unaona, unapoanza kumwombea mtu fulani, jambo fulani linaanza kutukia. Hapo ndipo tunaposhindwa, enyi marafiki, kutokuomba. Maombi ndiyo jambo la kimsingi. "Ombeni nanyi mtapokea. Hamna kwa sababu hamwombi; hamwombi kwa sababu hamwamini. Ombeni kwa wingi, kusudi furaha zenu zitimilike. Omba na uamini kwamba umepokea ulichoomba." Kisha ukishikilie. Usikiache. Kama ni ahadi katika Biblia, na imefunuliwa kwako ya kwamba Mungu atakupa, ishikilie.

101 Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwake—ilivyokuwa kwake. Ilifunuliwa kwake ya kwamba Zakayo wake ataokolewa, kwa hiyo alishikilia moja kwa moja.

102 Kwa hiyo wakati akianza kutoka mlangoni, akasema, "Zakayo, kwa nini umeamka mapema sana asubuhi ya leo?"

103 "Loo," akasema, "mpenzi, nilidhani ningeninii, en-he, en-he. . . " Mwajua, unaweza kutoa kila namna ya udhuru, Zakayo. "Nilifikiri ningetoka nje na kuvuta kidogo he—hewa safi. Unajua, kwa namna fulani . . . " Ungeweza kukisukuma huko kitu kama hicho, wajua? Naye akajua jambo fulani.

104 Kwa hiyo huyu hapa anatoka nje, akiangalia nyuma kwenye nyumba, mwajua, wakati akitoka kwenye ujia, akitazama nyuma. Mkewe akichungulia kupitia upenyo, mwajua, akiangalia aone aliyokuwa akifanya. Alijua papo hapo. Akaketi chini, akasema, "Asante, Bwana. Ninaamini yote yamekwisha sasa. Tumemfanya aanze kupiga hatua."

105 Kwa hiyo kama umemleta Zakayo wako mkutanoni asubuhi ya leo, yeye anapiga hatua. Huenda ameketi hapa, kwa hiyo anapiga hatua. Tumemfanya afikie umbali huo, kwa vyovyote vile.

106 Kwa hiyo akaanza kutoka, akiangalia nyuma, aone kama mtu yeyote alikuwa akimwangalia, mwajua. Akasema, "Sasa, unajua nitakalofanya?" Hebu tubadilishe mawazo yetu tuyaendee yake sasa. "Mke wangu amejiingiza sana katika hili, linaloitwa, Nabii wa Galilaya; wakati, ku—kuhani wangu na mchungaji wangu wanaponiambia, 'Hakuna kitu kama hicho siku hizi. Miujiza hii yote na kadhalika ni namna fulani tu ya hila za kudanganyia. Hamna kitu.' Unajua nitakalofanya? Ninashuka moja kwa moja niende huko na nimwelezee ukweli wa mambo. Bila shaka, na hilo litanifanya kuwa mtu maarufu sana katika mji huu, mnaona, wakati ninapoweza kumwaibisha, usoni Mwake. Nitafanya hilo." Kwa hiyo huyo anatoka anaenda.

107 Kasema, "Sasa Yeye ataingilia upande wa kusini, hapana, ama atatokea kaskazini, akiteremka kutoka Yerusalemu, Yeye, kutoka Dani hadi Bia-sheba, akiteremka." Kasema, "Nitaninii—nitaninii—nitaninii . . . Yeye anateremka chini kutoka Yerusalemu, kwa hiyo nita—nitateremka kule chini

kwenye lango la kaskazini. Nitamnasa wakati anapoingia. Nami nitasimama pale pale na kumwangalia vizuri, nami nitampa ukweli wa mambo."

108 Loo, ni Zakayo wangapi waliopo siku hizi, wanaozungumza juu ya Yesu mkutanoni, "Ni kundi la watakatifu wanaojifingirisha. Hamna kitu kwa hilo. Kama nikimnasa mtu huyo, nitakayofanya!" Unaona?

109 Kwa hiyo anateremka kwenda langoni. Lakini ajabu ni kwamba, unajua . . . Yeye alikuwa akienda kujipatia mahali fulani papo hapo langoni, amwambie yeye alikuwa ni mfanya biashara; alikuwa ni mwanachama wa Ki—Kiwanis, a—alikuwa ni mshirika wa mashirika na—na ninii vyote—vilabu vya wanawake mjini. Yeye, yeye alikuwa—alikuwa mmoja wa maafisa huko, na alikuwa mtu mashuhuri na aliyeheshimika. Alikuwa raia mwenye heshima. Naye kweli alitaka kumwambia haikumpasa kuingia kwenye mji huo, walikuwa na wahubiri wengi na makanisa mengi, hawakuhitaji mawazo yake kule. Kwa hiyo anashuka mtaani kwa mikogo, na kifua chake kidogo mbele, mwajua. Na, loo, jamani! Nini? Mbona, huenda rabi akamfanya shemasi kama wakifanya kitu kama hicho. Kwa hiyo anateremka kwenda langoni.

110 Lakini jambo la ajabu. Vema, unajua, kwa namna fulani ni jambo lisilo la kawaida, lakini, kila mahali ambapo—ambapo Yesu anatokea, kwa kawaida huwa kuna mtu pale kumsikiliza. Unaona? Na kabla hajafika pale, a—alisikia kelele. Nao walikuwa wakiimba kila aina za nyimbo, na—na, "Utukufu kwa Mungu aliye Juu Sana," na nyimbo hizi zote nzuri walizokuwa wakiimba, na wengine wakipiga mayowe na kupaza sauti. Si ni ajabu, alipo Yesu, daima pana kelele nyingi? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Unaona? Ni ninii tu . . .

111 Mwajua, Yeye aliingia hekaluni na . . . siku moja, kwenye, huko Yerusalemu, hasa, na, alipoingia, waliikata mitende, na kupaza sauti. Na hao hapo wamesimama, wale maprofesa mashuhuri wa mashirika na kadhalika, na makuhani, na kusema, "Watulize."

112 Akasema, "Wakinyamaza, miamba itapaza sauti mara moja." Unaona, kitu fulani kitalia wakati Yeye akiwako. Hiyo ni kweli.

113 Unajua, wakati Haruni alipoingia kwenye Shekina, mbele ya Shekina, ilibidi atiwe mafuta, naye alikuwa . . . mavazi yake ilibidi yawe na komamanga na kengele. Na hiyo ndiyo njia pekee waliyojua ya kwamba Haruni alikuwa angali hai, wakati walipoisikia sauti hii. Na wakati ninapowazia ya kwamba hiyo ndiyo njia pekee ambayo Mungu anajua kama sisi tuko hai au la, wakati unaposikia sauti kidogo. Hebu chukua kitu chochote kilichokufa kabisa, ambacho kilipatwa na jambo fulani. Kwa

hiyo iliwapasa kujua kama alikuwa hai ama la, kwa sauti iliyotoka.

114 Kwa hiyo Zakayo akasikia kelele hii yote huko chini. Na kwa hiyo wakati alipofika kule, malango yalikuwa yamejaa, na juu kwenye kuta, na kila kitu. Naye alikuwa ni maskini jamaa mdogo tu, haidhuru, kwa hiyo akawazia, "Nitamwonaje? Kutakuwako na wengi sana wa hao watakatifu wanaojifingirisha wamemzunguka, mpaka si—siwezi hata kumwona. Kwa hiyo mwajua," akasema, "Ninajua jambo moja, siwezi kumwona hapa, kwa kuwa mimi ni mdogo sana."

115 "Lakini najua Yeye anateremka huko chini kwa mshindani wangu kwa—kwa chakula Chake cha mchana. Kwa hiyo sioni, kama Yeye alikuwa ni Mtu mwenye akili, angekuja mahali pangu pa biashara, mkahawa wangu. Lakini anashuka kwenda kwa Lavinski." Ama, natumaini hakuna Lavinski hapa. "Kwa hiyo basi, kwa vyovyote vile, anaenda kwenye mkahawa wake. Na, kwa kweli, mimi huandaa chakula kilicho kizuri kuliko vyote, na—na kwa nini Mtu hata . . . na huku Rebeka akiwa ni mfuasi wa kanisa Lake, na halafu aende mahali kama hapo?"

116 Vema, akasema, "Ninajua jambo moja, nitashuka hapa ambapo Barabara Kuu ya Haleluya inapokingama Barabara ya Utukufuni. Yeye atapitia njia hiyo." Hiyo ni kweli. "Papo hapo, kwenye barabara ya mjini, ambapo Barabara Kuu ya Haleluya na Barabara ya Utukufuni zinapokingamana." Daima unaweza kumpata moja kwa moja hapo.

117 Kwa hiyo akauacha umati huo na kutimua mbio kule chini, naye akawaza sasa, akajitengeneza, na kusema, "Sasa Yeye atakapofika kwenye hiyo kona, nitamwambia, atanitambua. Atakuja kupitia njia hii, kwa hiyo ni—ni—nitaninii . . . atakapopitia hapa." Ndipo akaanza kuwaza, "Unajua nini, ule umati utamfuata."

118 Daima wanamfuata. "Palipo na mzoga, tai watakusanyika." Sio kuku, wale ndege wa ardhini. Tai wa mbinguni atakusanyika pamoja na mzoga. Kuku ni binamu yake, mnajua, yeye yupo hapa chini ambapo panya na kila kitu wanaweza kumla. Lakini tai huweka kiota chake huko juu kabisa mtini, hakuna mtu anayeweza kukifikia hicho. Kupe hawawasumbui; wanaruka juu sana. Sasa, wala nyama na panya na kadhalika hawatawasumbua, yeye ni tai. Wanapenda Chakula cha tai. Ndicho *Hiki*.

119 Mnajua, Yehova ni tai, Mwenyewe, na Yeye anatuita makinda wa tai. Manabii Wake ni tai, waonaji.

120 Tai huruka juu sana, hakuna ndege mwingine anayeweza kumfuata. Mbona, kama mwewe akijaribu kumfuata, atavunjika vipandevipande. Hiyo ni kweli. Hiyo ndiyo shida ya siku hizi, wengi sana wanajaribu kuigiza. Watatambua hivi karibuni. Hebu mwache aruke juu zaidi kidogo, manyoya yote

yatapukutika. En-he, en-he, a-ha. Kweli. Watashushwa chini. Kumbukeni, hana budi kuwa ni ndege aliyeumbwa kwa njia maalum. Naye mtu anayeweza kulifuata Neno hili hana budi kuwa ameumbwa kwa njia maalum, ameumbwa na Mungu, sio seminari. Tunaona wakati yeye . . . kadiri anavyoruka juu zaidi, kama manyoya yake hayatashikilia, itamfaa nini.

121 Na jambo lingine, wakati anapofika huko juu, vipi kama akifika huko juu naye ni kipofu na hawezi kuona kitu? Unaona, hana budi kuwa na macho pia (unaona?), kujua analofanya wakati akiwa huko juu. Ndivyo walivyo tai wa Mungu. Kadiri unavyopaa juu, ndivyo unavyoweza kuona mbali zaidi, unarudi na kutabiri yale yanayokaribia kutukia. Mnaelewa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Nafikiri yule ndugu mweusi huko nyuma anaweza kuelewa hilo vizuri sana asubuhi ya leo, mnaona. Sasa angalieni.

122 Ndipo tunaona ya kwamba Yeye alisema, "Kama nikisimama hapa, kundi lile lile la makelele, kamwe Yeye hataisikia sauti yangu. Wanapaza sauti na kufanya yasiyofaa kwa hiyo, shutuma langu Kwake halitamaanisha lolote." Hilo ni zuri. Kwa hiyo basi akasema, "Lakini unajua nitakalofanya? Nitakwambia nitakalofanya. Upo mkuyu unaosimama hapa. Nami nitaupanda mkuyu huo, ndipo atakapopitia njia hii, nitamwona. Halafu nitatoka moja kwa moja pale kwenye moja la hayo matawi, nami nitamwambia kile ninachotaka kumwambia. Ndipo atajua ya kwamba mimi ni Zakayo, mfuasi wa dhehebu hili zuri hapa chini. Nitamwambia kuwa mimi ni wa wapi na yale kuhani wangu anayomwazia." Vema, huenda hilo likawa ni sawa.

123 Anaangalia kila mahali, ndipo akawazia, "Sasa, jambo la pili, tawi la kwanza liko karibu—karibu futi kumi juu." Naye ana urefu wa takriban futi nne tu, kwa hiyo atapataje futi zingine sita? Mnaona? Kwa hiyo anashangaa jinsi angeweza kupanda kule juu. Hakuna njia nyingine ya yeye kulifikia, naye ingemlazimu kuupanda mti huu. Hivyo basi anaangalia kote, na hakuna kitu ila . . . Mwajua, uokotaji wa takataka ulikuwa haujafanyika bado asubuhi hii, na mapipa ya takataka yalikuwa yamewekwa pale pembeni. Yeye akawaza, "Laiti ningaliweza kulileta lile pipa la takataka hapa, kisha nininii . . . hiyo ingenifanya mrefu vya kutosha kufikia pale juu na kulishika lile tawi la kwanza. Lakini nimekusudia kumwona. Nitamwona."

124 Mwajua, kuna jambo fulani kulihusu, mtu anapotaka kumwona Yesu, yeye hupitia kwenye baadhi ya mambo magumu sana. Mnaona? Lakini, mnaona, Mungu alikuwa akimshughulikia. Ilikuwa ni kitu gani? Maombi ya Rebeka yakijibiwa, mnaona.

125 Vema, yeye anaenda huko. Naye mkusanya taka hakuwa amefika bado asubuhi hii, nalo pipa hilo lilikuwa ni zito sana,

kwa hiyo asingeweza kuliinua. Alikuwa ni mdogo sana. Kwa hiyo akajaribu, na asingeweza kuliinua. Kulikuwako na njia moja tu angaliweza kufanya hivyo, hiyo ni kulishika kwa mikono yake, alinyanyue. Lakini amevaa vazi lake lililo zuri kuliko yote.

126 Bali kuna jambo fulani kuhusu jambo hilo, wakati unapotaka kumwona Yesu sana, utafanya lolote. Mnaona? Uta—utafanya tu lolote, kama una hamu sana ya kumwona. Kwa hiyo anatoka anaenda huko nje na yeye . . . Unaona, Shetani atajaribu kukuzuia kufanya hilo, pia. Kila kitu, ataweka . . . Ataweka dosari njiani, kila wakati, kukuzuia usimwone. Atayapofusha macho yako kwa chochote awezacho. Lakini kama umekusudia, Mungu atakufanyia njia. Yeye anapitia njia hii asubuhi ya leo, pia. Usimwache Shetani aweke kitu fulani njiani mwako, "wakati wako, na *hili*, na sina budi kufanya *hili*." Kaa tu kimya kwa dakika moja.

127 Kwa hiyo anashuka pale, anainama, amevaa lile vazi zuri. Kwa kweli anajichafua sasa. Anaishika ndoo hii ya taka. Mara tu anapoishika na kuanza kuibeba, hawa hapa washindani wake wanapiga kona.

128 Ni karibu kama ilivyo hapa, ewe Zakayo. Ulisema kamwe usingeweza kuingiana na kundi la watakatifu wanaojifingirisha, lakini wewe huyu hapa.

129 Vema, huyu hapa ameketi, amesimama hapa sasa na ndoo hii ya taka, uso wa—wake mwekundu. Vema, mshindani huyu alisema, "Vema, angalia, yule pale Zakayo, yule mwenye mkahawa hapa chini, amebadilisha kazi yake. Ana cheo kipya. Vema, mnajua, yeye ni—yeye ni . . . anafanya kazi ya mji, kuokota takataka." Vema, kuna kitu fulani kingine juu yake, hata hivyo, kama umekusudia kumwona Yesu, utafanya lolote. Yeye aliishikilia tu, nao uso wake ukawa mwekundu, uso wake ukavimba. Naye huyu hapa anaenda, moja kwa moja pale na kuiweka chini. Anaangalia kote, anaacha wapige kona.

130 Ndipo anapanda juu ya lile pipa, na kuuparamia mti. Loloo, samahani, sikupaswa kusema hivyo. Kuparamia, mwajua, huko—huko ni . . . Ni wangapi wanaojua "kuuparamia mti" ni kitu gani? Vema, hilo ni sawa basi. Mnaona, kwa maneno mengine, anapanda juu ya mti.

131 Naye anafika kule juu, naye yule pale, ameketi pale. Nena kuhusu machafuko! Amejaa takataka, amechafuka kwelikweli.

132 Na, wakati mwingine, Mungu anakuacha tu uwe hivyo. Amina. Nilimsikia mtu fulani leo, mnajua njia yao mpya? Ninatumaini kamwe haitaingia kwenye mazingira yetu ya kipentekoste, ingawa ninaiona ikivuja na kumiminika ndani; kuingia, kupeana mikono, "Na—namchukua Yesu kama Mwokozi wangu." Ninapenda kuwaona wakishuka pale madhabahuni, na kufa, kupigwa, na kuugua, na kutoa udenda. Na, mwajua, wakati unaponinii . . . Tulikuwa na baadhi ya

farasi, na wakati tulipowalisha klova, ile klova nzuri kweli, tamu, iliyo na asali, iliwafanya kutoa udenda. Unapokaribia Kanaani vya kutosha, utatoa udenda kidogo, pia, mwajua, kwa kula hiyo Asali kutoka Kanaani.

133 Kwa hiyo tunaona ya kwamba huyu hapa, juu ya mti sasa, akijipanguza takataka kutoka kwa ninii yake mpya... Hakuwazia angefanya hivyo. Acha tu mtu aanze kukuombea, utafanya mambo yasiyo ya kawaida. Naye anaipanguza namna *hiyo*; na vibanzi kote magotini mwake na kote mikononi mwake, ameketi pale akivichokoa. Akasema, "Vema, sasa, kweli mimi ni mchafuko mtupu! Mimi huyu hapa nimeketi." Kasema, "Unajua, Rebeka aliniambia jamaa yule alikuwa ni Nabii. Sasa, ni—nitangojea, nitajificha." Kwa hiyo akaketi chini ambapo matawi mawili yanakutana, panakuwa ni mahali pazuri pa kuketi.

134 Na baada ya kufika umbali huo, nawe umefika umbali huu asubuhi ya leo, Zakayo, umeketi, pia, mahali ambapo njia mbili zinakutana, yako na ya Mungu. Unaona? Wakati ulipojitolea vya kutosha kuja huku asubuhi ya leo, vema, maombi ya Rebeka yako karibu kujibiwa. Lakini umeketi mahali njia mbili zinapokutana sasa, yako na ya Mungu. Unaona?

135 Basi akaketi pale, akawaza, "Alisema, 'Yeye ni nabii.' Mambo haya yote, 'Angeweza kuwaza mawazo ya mioyo ya watu, na kuwafunulia, na kuwaambia shida yao ilikuwa ni nini.' Na, loo, jambo hili kuhusu 'Nathanaeli, alikuja akamwambia yeye alikuwa chini ya mtini huko nje.' Mwajua, sitabahatisha. Nitajifunika, hapa juu mtini. Kwa hiyo niko ndani ya mti, pia. Na kwa hiyo siamini Yeye ni nabii, hata hivyo. Siamini kabisa, maana kuhani wangu ananiambia hakuna kitu kama manabii. Hatujakuwa nao kwa mamia ya miaka."

136 Kwa hiyo sasa, bila shaka, unatambua ninafanya mchezo wa kuigiza hapa, nipate kueleweka.

137 Kwa hiyo anashika matawi yote na kujizungushia, kila mahali, akajificha vizuri kabisa. Kasema, "Sasa atakapopita kwenye Barabara Kuu ya Haleluya, kutoka Haleluya aingie ya Utukufuni. Kwa hiyo papa hapa pembeni, atakapopitia pale, atakapopiga kona, nitajiachia jani moja kubwa hapa, kusudi niweze kuangalia na kumwona. Nitaliinua juu. Kamwe hataniona, si hapa juu. Na ndipo atakapokuja kupitia hapa, nami nimwangalie vizuri, mnajua nitakalofanya? Nitavuta matawi haya nyuma, na baada ya Yeye kupitia hapa, ndipo nitamtupia maneno makali. Atanitambua." Kwa hiyo akaketi pale kwa muda kidogo.

138 Baada ya kitambo kidogo akasikia kelele ikija. Kwa kawaida Yesu huja na kelele hizo. Kwa hiyo huyu hapa anapiga kona. Hivyo, yeye, jambo la kwanza analopata ni lipi? Kundi la watu likikusanyika mitaani. Akasema, "Nina furaha nipo hapa juu kwenye mti huu, kwa hiyo sitachangamana nao tena."

Kwa hiyo huyu hapa juu ya mti, ameketi pale, amejificha kabisa, kusudi asitambulikane na mtu yeyote, washindani wake hawatajua yuko juu ya mti sasa. Kwa hiyo ana jani hili moja tu ambalo ataliinua na kuchungulia, na kulirudisha tena, na sehemu zingine zote za mwili wake zimefunikwa kabisa. Kwa hiyo akainua hilo jani, nao watu wanakusanyika pembeni.

139 Na, mwajua, huyu hapa Bw. Jones anakuja na huyo mtoto mgonjwa. Wakati aliposikia ya kwamba ku—kuhani na daktari, moja kwa moja mkahawani mwake, wakilizungumzia hivi majuzi, kwamba, "Mtoto huyo alikuwa anakufa, alikuwa na homa ambayo daktari alijaribu kuitibu, wala hakuna kitu kingaliweza kuitibu. Na huyo mtoto hapaswi kabisa kutoka kwenye hiyo nyumba. Lakini hapa, yule," mteja wake mwenyewe, "amekuwa mshupavu sana mpaka wakamleta mtoto huyo huku nje kwenye upepo huo baridi wa Marchi. Nao hapa walikuwa wamemfunika kwa blanketi, msichana mdogo wa takriban miaka kumi. Ni mshupavu jinsi gani! Atakapoingia kwenye mkahawa wangu tena, mtoto huyo atakuwa amekufa, bila shaka; nitamwambia, atanitambua!"

140 Baada ya kitambo kidogo kelele inaongezeka zaidi na zaidi, nao wote wanakimbia barabarani. Kitu cha kwanza kufika kona ya Barabara Kuu ya Haleluya, kufikia kona ya ile ya Utukufuni; wanapopiga kona barabarani, tunaona, yupo mvua samaki mkubwa mno mkakamavu, jina lake Simoni, akisema, "Mwaweza kusonga kando, jamani?" Hawa hapa kumi na mmoja zaidi nyuma yake, wakisema, "Tunaomba, tafadhalini, songeni kando. Bwana wetu alikuwa kwenye ibada kubwa jana jioni, na—na nguvu zilimtoka, na maono makubwa yakatokea. Naye amechoka asubuhi ya leo, na Yeye—Yeye—Yeye anaenda kula kiamshakinywa. Mwaweza kusonga kando, tafadhalini?"

141 Nayo hii hapa familia ya Jones inatoka nje, pamoja na huyu mtoto. Ndipo yule mvua samaki mkubwa na wengine wengi, wakasema, "Samahani, rudini nyuma, tafadhalini." "Vema, tuna mtoto hapa ambaye kweli atakufa tu. Madaktari wamemkatia tamaa. Naomba uturuhusu angalau kumweka mtoto huyu . . . "

142 "Samahani. Wote watataka kufanya hivyo, kwa hiyo kamwe si—siwezi kufanya hivyo. Itawabidi kusimama mbali, hapo kando. Yeye anakuja sasa hivi. Hivi mwaweza kusonga nyuma tafadhali?"

143 Kwa hiyo ninaweza kuona basi, kama maskini yule mlinzi, kutoka kwenye mnara alimokuwa, mtini, akiangalia, ndipo akamwona Bw. Jones na Bibi Jones wakipiga magoti, kwenye umati huo, kasema, "Bwana Mungu, usinipite. Ee Mwokozi mpole, sikia kilio changu kinyenyekevu. Unapowaita wengine, usinipite."

144 Ndipo alipokaribia, alisimama, na kusema, "Bw. Jones, waweza kumleta mtoto wako hapa?" Kwa namna fulani lilikuwa la kusadikisha.

145 Ni yeye yule leo. Haihitaji kadi ya maombi. Haihitaji kundi. Inahitaji imani, kama ile kipofu Bartimayo aliyokuwa nayo upande ule mwingine mwishoni mwa lile lango wakati Yeye alipotoka. Yadi mia mbili kutoka Kwake, ulikuwa ndio umbali wa mahali hapo, Yeye angaliwezaje kuisikia sauti yake? Lakini, "Ee Yesu, Mwana wa Daudi," hilo likamsimamisha, akaligusa vazi Lake. Ndipo akageuka, kasema, "Mleteni hapa." Mnaona?

146 Nao wakamleta huyo mtoto mchanga pale. Akaweka mikono Yake juu ya maskini mtoto huyo mchanga, hayo tu ndiyo aliyofanya. Katika dakika chache, babaye akamchukua tena, naye mtoto huyo akashuka mtaani, akikimbia mbio. Homa ilikuwa imemwacha.

147 Kwa namna fulani lilimpoesha kidogo. Akasema, "Nashangaa kama Yeye angekuwa ni Nabii?" Kidogo lilimfanya aamini hilo.

148 Unajua, kuna mambo kama hayo yanayotushawishi, kwa kuwa Yeye ni Neno, (sio "Nilikuwa"), "MIMI NIKO."

149 Na wakati anapofika chini ya ule mti, akawaza. . . Vema, analiinua jani hili dogo juu, akichungulia chini. Alipofika chini ya ule mti, akawaza, "Hivi Yeye anaweza akawa ni nabii? Huenda ikawa." Mnaona, huna budi kuwa na imani. "Anaweza kuwa?" Na wakati akipitia chini ya mti ule, amekiinamisha kichwa Chake, akitembea kwa njia Yake ya upole.

150 Kuna kitu fulani kingine, wakati wowote ukipata kumwona Yeye, u—u—unabadilishwa. Huwezi kuwa vile vile tena. Nilisikia juu Yake, ulisikia juu Yake; lakini wakati nilipomwona, Neno Lake, kamwe ni—ni—nisingeweza kuwa vile vile tena. Kuna jambo fulani kumhusu, tofauti na watu wengine. Kuna jambo fulani kumhusu Yeye, tofauti na maaskofu na makadinali na mapapa, na kadhalika. Yeye, kuna jambo fulani kumhusu ambalo ni tofauti.

151 Maskini Zakayo alikuwa ameguswa. Maombi ya Rebeka yalikuwa yamejibiwa. Akipitia chini ya ule mti, alisema, "Vema, hu—huenda nikamwomba radhi Rebeka nitakaporudi. Yuko njiani akienda kwa Lavinski, hilo ni sawa. Kama akila kwenye mkahawa mwingine, ni sawa kwangu sasa." Mnaona, yeye alikuwa amemwona tayari.

152 Kwa hiyo wakati alipofika papo hapo chini ya mti, alisimama, akatazama juu, kasema, "Zakayo, shuka chini. Ninaenda nyumbani pamoja nawe, kwa mlo mkuu wa kutwa leo hii." Unaona, Yeye alijua alikuwa huko juu. Alijua alikuwa ni nani.

153 Ndugu, dada, ni Yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye anakuja kupitia njia hii asubuhi ya leo. Amepitia njia hii katikati ya mji, amekuwa hapa pamoja nasi juma hili.

154 Mnajua nini? Kama Rais alikuja, Rais Johnson alikuja Topeka, bendera zingekuwa zikipepea, barabara zingepambwa, naye angekaribishwa kwa shangwe. Lakini Yesu anaweza kuja, ni vigumu kumpata mtu anayetaka kuja kumwona. Ingekubidi kupata ulinzi wa polisi kumleta Rais kwenye mji huu, bali tuna nafasi tele ya watu kuketi. Mnaona tofauti yake? Hawashughuliki kumwona Yeye.

155 Natumaini Zakayo yupo hapa asubuhi ya leo. Na wakati anapopitia njia hii, huyo ni Yeye anayekuzungumzia.

156 Akashuka kutoka mtini. Hakika, wakosoaji walitaka kusema, "Mtu huyu ni mwenye dhambi."

157 Yeye alisema, "Bwana, kama nimechukua chochote kwa njia ya udanganyifu, nitakirudisha mara mia moja. Nitakirudisha. Na kama nimemlaghai mtu yeyote, niko tayari kulisahihisha. Ni—niko tayari."

Na tuviinamishe vichwa vyetu.

158 Zakayo, uko tayari asubuhi ya leo? Kwa nini usishuke sasa kutoka mtini? Mbona usije? Yeye anapita njia hii sasa, akipitia moyoni mwako, akisema nawe. Kungekuwako, wakati umekiinamisha kichwa chako, ukiomba, kuna mtu yeyote hapa angetaka kusema, "Ndugu Branham, kweli kidogo nimekuwa nikishuku tangu zamani"? Kumbukeni, yeye alikuwa ni mtu wa dini, yeye mwenyewe. "Nimekuwa kidogo tu ni mwenye kushuku, lakini sasa ninaamini. Saidia kutokuamini kwangu, Mungu." Sio kwa Ndugu Branham, maana hakuna mtu anayeangalia ila mimi na Mungu, "kwa hiyo nitainua mkono wangu na kusema, 'Usinipite, Ee Mwokozi mpole. Kisikilize kilio changu kinyenyekevu. Nifanye mwaminio wa kweli, Bwana. Njoo, nenda pamoja nami nyumbani leo hii na ukae nyumbani mwangu.' 'Leo lazima nishinde nyumbani mwako.'"

159 Utainua mkono wako, useme, "Nikumbuke, Mungu"? Bwana akubariki, akubariki, na wewe. "Unikumbuke, Mungu. Nenda nyumbani pamoja nami, asubuhi ya leo. Ninajua upo hapa. Ninajua unaujua moyo wangu. Unanena nami sasa. Unajua mambo ambayo nimefanya ni mabaya. Unajua mimi hata ni mfuasi wa kanisa la full Gospel, lakini hata hivyo nimekuwa mzembe, sijafanya kilicho chema. Nimepuuza mkutano wa maombi. Nimeweka kitu kingine chochote . . . Nimefanya mambo, kweli, ambayo—ambayo hayaambatani na imani yetu."

160 "Mimi—mimi ni—mimi ni mwanamke, nami ninajua nimevalia vibaya. Pia nimezikata nywele zangu. Nimejipodoa. Na ninapaswa kuwa ni mwanamke wa full Gospel, dada. Nirehemu, Bwana. Ni—ninataka uende nyumbani pamoja nami leo hii, na ni—ni—nitakuwa m—mfano ulio hai wa Kristo,

tangu sasa na kuendelea." Ungeweza tu kuusikia huo Uwepo wa Mungu, kwamba ungeinua mkono wako, na kusema, "Niombee." Mungu akubariki, na Mungu akubariki, wewe. Mungu awabariki, enyi dada. Naam.

161 Baba wa Mbinguni, baadhi ya akina Zakayo wadogo na Zakayo wakubwa wameliinua jani na kuchungulia. Wametambua ya kwamba Yesu amepata mahali wanapoishi na mahali walipo, amewafunulia kwamba wamekosea. Mikono mingi, mingi sana humu ndani imeinuliwa. Naomba uende pamoja nao nyumbani leo, Baba, uende nyumbani mwao, ukaishi mioyoni mwao. Jalia wasiisahau asubuhi hii. Hata hivyo, katika ninii...mambo ya dhihaka ambayo mimi... na kujaribu kulimbikiza hi—hi—hisia ya ucheshi kati ya umati uliochanganyikana. Na sasa katika wakati huu ambapo jambo lenyewe limejitokeza, ya kwamba ni—ni la kuninii tu—kuwafanya watu watambue kile kinachosimama nasi hapa asubuhi ya leo, Neno likidhihirishwa mjini mwetu, miongoni mwetu, Bwana Yesu Mwenyewe, Neno lililofanyika mwili, akitenda kazi Mwenyewe kwa mwili wa mwanadamu. Ee Mungu, jalia marafiki wetu wapendwa waone jambo hili na waletwe karibu na Wewe.

162 Nenda nyumbani pamoja nao, ninaomba tena, Baba, pamoja na kila Zakayo na kila mwanamke, kila Rebeka. Jalia ajue ya kwamba maombi yake yamejibiwa. Tunawakabidhi Kwako sasa. Na wajalie, bila kusitasita, wakukubali moyoni mwao, kama vile maskini Mwebrania huyu alivyofanya asubuhi ile, ingawa walikuwa wamekosea. Kasema, "Hivi si inampasa na Yeye pia, akiwa ni mwana wa Ibrahimu." Kwa hiyo Wewe uko tayari kwenda nyumbani pamoja nasi, Baba. Tunaomba ya kwamba kamwe hutatuacha. Nenda pamoja nasi, kutoka kwenye kiamshakinywa, tunapoketi hapa asubuhi ya leo; na tumeangaliana mezani sisi kwa sisi, wenye furaha, wenye vichekesho, tukipeana mikono, na tukipendana sisi kwa sisi, kama vile Wakristo tu wanavyoweza kuwa.

163 Nami nafikiri huenda ni—ni—nisiwe hapa tena. Huenda ni—nisikutane na kundi hili tena namna hii, kwenye kiamshakinywa kingine. Lakini nina hakika, Baba, kama watakuruhusu tu kwenda nyumbani pamoja nao, leo, na kukaa pamoja nao, nitakutana nao kwenye ile Karamu, wakati ushindi utakapopatikana kabisa nayo meza kuu itandaziwe kitambaa cha mbinguni, nasi tuketi na kuangalia upande wa pili.

164 Nami ninawaangalia asubuhi ya leo wahudumu walioketi hapa, wenye mvi, waliokuwa wakihubiri nilipokuwa mvulana. Nafikiri walikatilia mbali visiki tu, wakazilipua barabara, wakaifanya ya kutumika kwa urahisi kwa karama hizi ambazo walitabiri zitakuja. Mungu, wabariki, wabariki wote. Wabariki wanawake hawa wazuri waliojitolea kusudi waume wao wapate

kuhubiri, na kujitolea mhanga ambako Wakristo wote kweli hujitolea. Kuwa pamoja nao, Baba.

165 Tuketi pale usiku huo, tukiangaliana mezani, na labda kamwe hatutaonana tena tangu asubuhi ya leo, hadi wakati huo. Lakini, hapana shaka, machozi pia yatatiririka mashavuni mwetu, kwa furaha, wakati nitakaponyosha mkono mezani na kuwapa mkono. Ndipo tutamwona akitoka. Tutafurahi sana tulishuka kutoka kwenye ule mti, labda mti wa kanuni za imani, mti wa kanuni za imani za kimadhehebu, ama kitu fulani, kutoka tu kwenye uchoyo wetu, kutoka kwenye njia zetu za kijinga, ama kutokumjali kwetu; tutoke kwenye upofu wetu, tuingie Nuruni. Tutakuwa na furaha kuhusu jambo hilo wakati huo tutakapomwona akitoka, amevaa mavazi Yake yote ya Kifalme, ashuke aje mezani, na kuuchukua mkono Wake wa thamani na kupangusa machozi yote kutoka machoni mwetu, aseme, "Msilie. Yote yamekwisha. Ingieni katika furaha za Bwana, mlizoandaliwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu." Mpaka wakati huo, Baba, kaa pamoja nasi, nenda nasi nyumbani na ukae pamoja nasi, mpaka kwenye saa hiyo. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

166 [Dada mmoja ananena kwa lugha nyingine. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Nampenda, nampenda
Kwani . . . kwanza

167 Wakati nilipopanda mtini, Yeye angali alinipenda.

Na kunu- . . .

Angalia ni mti wa jinsi gani Yeye alioupanda kwa ajili yangu, Msalaba, mti uliodharauliwa.

Mtini Kalvari.

168 Angalia ni mti wa aina gani alioupanda, apate kukutoa kwenye mti wako.

Na . . .

169 Sasa, hamwezi kumpenda Yeye pasipo kupendana ninyi kwa ninyi.

Na . . .

Sasa nyosha mkono mezani, na kusema, "Mungu akubariki, msafiri," mfikie tu mtu fulani upande wa pili.

Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

170 Hivi humpendi kwa sababu alienda kwenye ule mti kwa ajili yako, apate kukutoa kwenye mti wako? Hivi hutamruhusu aende pamoja nawe nyumbani asubuhi ya leo? Ni wangapi watakaomchukua? Inua mkono wako. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mungu awabariki.

171 Wafanya Biashara, ninataka kuzungumza nanyi kwa dakika moja, kabla ya kuondoka.

172 Sasa kama wewe si Mkristo, kama hujawa ukijihusisha; ninyi Wakristo, ninyi watu, kama ulimkubali Kristo wakati ulipoinua mkono wako, nenda kwa mmoja wa wachungaji hapa, waambie kile umefanya. Watawapokea. Mtu fulani ama mchungaji aandike barua ya huyu, kwa huyu mvulana hapa, huyu ndugu mweusi. Hiyo ilikuwa ni neema jana usiku, yule kijana mwanamume anayeketi pale akiangalia hilo na akaamini hilo. Mnaona? Mnaona hilo? Jinsi ambavyo mvulana huyo, jinsi ambavyo huyo Roho alivyogeuka. Billy alikuwa akiniambia kulihusu, na mke wangu na hao wengine, baada ya sisi kufika nyumbani. Akageuka wakati alipokuwa amefika hapa pembeni, akarudi na kumpata yule, mnaona, kumleta nyumbani. Ukuu! Wewe nenda pamoja Naye. Nenda ukajiunge na kundi fulani mahali fulani ambalo unaweza kushiriki pamoja nalo, linalohubiri Neno lote la Mungu. Na udumu na hilo Neno, haidhuru, unaona. Hiyo ni kweli.

173 Mfanya Biashara, ulijua kilichompata Zakayo? Yeye alijiunga na Wafanya Biashara wa Full Gospel wa Yeriko. Hiyo ni kweli. Hilo tawi huko chini, alikuwa ni mshirika wake. Linasikika ni la kijinga, bali ni kweli namna hiyo. Nina hakika Yesu asingeanzisha chochote ila tawi la Injili yote, naye Zakayo akawa pamoja Naye. Kwa hiyo sasa, Zakayo, wewe fanya jambo lile lile.

174 Mpaka tutakapowaona usiku wa leo, Mungu awabariki. Nitamrudishia mchungaji ibada hii hapa.

Yesu Ni Nani? SWA64-0620B
(Who Is Jesus?)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi asubuhi, tarehe 20 Juni, 1964, kwa ajili ya kiamshakinywa cha Ushirika wa Kimataifa wa Wafanyabiashara wa Full Gospel katika Holiday Inn huko Topeka, Kansas, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2017 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org